

**CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN  
AFRICA**

**P. O. BOX 62157,  
NAIROBI - KENYA**

**TELEPHONE 891601, FAX 254-2-891261**

**REVISED BACHELOR OF EDUCATION DEGREE  
KISWAHILI PROGRAMME**

This Proposal was approved  
by the Commission for  
Higher Education on  
30/06/2008  
*AKenge*  
AUTHORISED SIGNATURE

*Submitted to  
The Commission for Higher Education  
Nairobi, in June 2005*

## 2.0 SHAHADA YA KWANZA KATIKA KISWAHILI

### 2.1.0 Mpangilio wa Somo

Filosofia ya kufunza shahada ya Digrii ya Lugha ya Kiswahili:  
Kozi ya Shahada ya Lugha ya Kiswahili imeanzishwa na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki ili kuendeleza lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya kimataifa katika nchi nyingi za eneo la Afrika Mashariki na Kati. Kozi hii ina madhumuni ya kuwatayarisha wataalamu wa lugha hii walio na maadili na ambao watahudumu katika nyanja mbalimbali za lugha hii kama vile uandishi, utafiti, ufundishaji, utangazaji na kadhalika.

### 2.1.1 Mahitaji ya Digrii

### 2.1.2 Masharti ya Usajili

- a) Masharti yanayohusu digrii za kwanza katika chuo kikuu yatatumika.
- b) Masharti yanayohusu digrii za kwanza katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii yatatumika.
- c) Idara itasajilisha:
  - i) Wanafunzi walio na alama ya C katika Kiswahili katika mtihani wa KCSE au kiwango sawa na hicho watasajiliwa katika kozi ya kipindi cha miaka minne;
  - ii) Wanafunzi walio na 'principal' katika Kiswahili katika mtihani wa "A level" au kiwango sawa na hicho watasajiliwa katika kozi ya miaka mitatu.

Au,

Astashahada ya P1 katika ualimu yenye pointi zisizozidi 28, pamoja na gredi ya jumla isiyopungua C na alama isiyopungua C katika Kiswahili katika mtihani wa Kenya Certificate Secondary of Education (KCSE) au kiwango sawa na hicho.

- iii) Wanafunzi walio na stashahada katika Elimu au kiwango sawa na hicho, na Kiswahili kama somo la kufundisha, watasajiliwa katika kozi ya miaka miwili.

